TANGAZO LA SERIKALI NA. 712 la tarehe 28/8/2020

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA MIJI)

SURA 288

# SHERIA NDOGO

*(Zimetungwa chini ya Kifungu cha 89)*

## SHERIA NDOGO ZA AFYA NA USAFI WA MAZINGIRA ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA MPANDA ZA MWAKA 2020

Jina

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za Afya na Mazingira za Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda za Mwaka 2020.

Tafsiri

2. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa itakapoelezwa vinginevyo: -

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote atakayeteuliwa na Halmashauri kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

"chakula" maana yake ni kitu chochote kinacholiwa au kunywewa na binadamu isipokuwa dawa, hii ni pamoja na: -
(a) kitu chochote kinachotumika katika matengenezo ya chakula;
(b) kitu chochote kinachoongeza ladha ya chakula; au
(c) kitu chochote kinachobadili rangi ya chakula;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda;

Sura ya 191

"kaya" maana yake ni familia inayojumuisha baba, mama, mtoto au watoto na mtu mwingine yeyote anayeishi na familia hiyo au watu wanaokaa katika nyumba moja na kuishi kama familia au mtu yeyote anayeishi peke yake katika chumba au nyumba;

"maji taka" maana yake ni ile iliyoainishwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira;

"mkazi" maana yake ni mtu yeyote anayeishi katika

eneo la Halmashauri na ambaye ana kaya au anaishi katika kaya au taasisi iliyopo katika eneo la Halmashauri au anafanya biashara katika eneo la Halmashauri;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri pamoja na Afisa yeyote atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"taka" maana yake ni ile iliyoanishwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira;

"taka ngumu" Maana yake ni ile iliyoainishwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira;

"Wakala" maana yake ni mtu binafsi au kikundi cha watu, kampuni, taasisi au shirika aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi.

Wajibu wa kufanya usafi wa mazingira

3. (1) Kila mkazi anayemiliki eneo la nyumba, kiwanja au biashara au atakuwa na wajibu wa kuhakikisha kwamba anafanya usafi wa mazingira yanayozunguka makazi au eneo lake hadi mwanzo wa mipaka ya barabara ya mbele ya nyumba yake.

(2) Kila mmiliki wa nyumba, kiwanja au eneo la biashara atakuwa na wajibu wa kuondoa uchafu kama vile mchanga, majani, nyasi au vitu vingine vinavyofanana na hivyo kwenye mifereji ya kupitisha maji inayozunguka au kupita kando ya nyumba, kiwanja au eneo la biashara yake.

(3) Bila kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1), na cha (2) kila mkazi atakuwa na wajibu wa kushiriki katika shughuli za usafi wa mazingira katika kila jumamosi ya mwisho wa mwezi au katika siku itakayopangwa na Halmashauri.

(4) Mtu yeyote atakayekiuka masharti ya kifungu atakuwa ametenda kosa.

Wajibu wa kuondoa na kudhibiti mazalia

4. (1) Mmiliki wa nyumba, kiwanja au eneo la biashara atakuwa na wajibu wa kuhakikisha kuwa katika

ya mbu.

eneo lake hakuna mkusanyiko wa maji, maji machafu, takataka au kitu chochote cha majimaji au kigumu ambacho kinaweza kuruhusu kuwepo kwa mazalia ya mbu au wadudu wengine wenye madhara kwa afya ya binadamu.

(2) Mtu yeyote ambaye bila sababu za msingi, atakiuka masharti ya kifungu kidogo cha (1) atakuwa ametenda kosa.

Upulizaji dawa

5. (1) Mtu yeyote anayeendesha biashara ya upuliziaji dawa ya kuuwa wadudu au wanyama waharibifu katika eneo la Halmashauri atatakiwa:

(a) kuwa na cheti cha taaluma kinachotambuliwa na Serikali na leseni hai kutoka Halmashauri;
(b) kusimamiwa na Afisa Afya wakati wa upulizaji; na
(c) kutoa cheti baada ya kupuliza dawa kilichosainiwa na Afisa afya.

(2) Mtu yeyote atakayekiuka masharti ya kifungu kidogo cha (1) atakuwa ametenda kosa.

Matengenezo na maegesho ya magari, pikipiki na mitambo

6. (1) Matengenezo ya magari, pikipiki na mitambo yatatakiwa kufanyika kwenye karakana, gereji au maeneo yaliyoruhusiwa baada ya kupata kibali rasmi kutoka Halmashauri.

(2) Mtu yeyote:

(a) hatoruhusiwa kutengeneza gari, pikipiki au mtambo wowote katika eneo la makazi, eneo la wazi au eneo ambalo halikutengwa kwa shughuli hiyo;
(b) kuegesha gari bovu kwenye njia ya miguu, mtaa, uchochoro, mtaro, maeneo ya wazi au barabarani.

(3) Mtu yeyote atakayekiuka, bila sababu za msingi, masharti ya kifungu kidogo cha (2) atakuwa ametenda kosa.
.

Utengenezaji, na uuzaji vyakula.

7. (1) Mtu yeyote anayetengeneza, kuchoma, kupika, kuchemsha au kuuza chakula cha aina yoyote katika eneo la Halmashauri atatakiwa:

*Tangazo la Serikali Na. 712 (Linaendelea)*

(a) kutimiza masharti na kanuni za afya; na
(b) kuwa na kibali kutoka kwa Afisa Afya wa Halmashauri.

Machinjio na maduka ya nyama

8. (1) Mtu yeyote hatoruhusiwa;
(a) kuchinja mifugo katika maeneo yasiyokuwa machinjio;
(b) kuuza nyama ya aina yoyote katika maeneo yasiyokuwa maduka ya nyama au katika maeneo yasiyoruhusiwa na Halmashauri;
(c) kuuza nyama isiyokaguliwa na mtaalamu wa mifugo au mtaalamu wa afya; na
(d) kusafirisha nyama kwa madhumuni ya kibiashara toka machinjioni bila kutumia gari maalumu la kusafirishia nyama lililoidhinishwa na Halmashauri.

(2) Kila mmiliki wa duka la kuuzia nyama atatakiwa kuhakikisha yafuatayo:
(a) duka lake ni jengo la kudumu lililosakafiwa kwa marumaru nyeupe hadi urefu wa futi sita kutoka usawa wa sakafu;
(b) duka lake lina maji safi, misumeno ya kukatia nyama na vyuma vya kutundikia nyama;
(c) duka lake lina kabati la vioo na jokofu la kuhifadhia nyama na mizani ya kupimia nyama;
(d) duka lake lina pipa au kifaa cha kuhifadhia takataka;
(e) muuzaji ana vazi jeupe pamoja na aproni nyeupe na kofia nyeupe;
(f) muuzaji anapima afya kila baada ya miezi sita; na
(g) duka lake lina karo la maji machafu.

(3) Mtu yeyote atakayekiuka masharti ya kifungu kidogo cha (1) na (2) atakuwa ametenda kosa.

Uendeshaji wa biashara ya hoteli na hosteli

9. (1) Kila mmiliki wa nyumba ya kulala wageni, hosteli, shule, kituo cha kutolea huduma za afya au nyumba ya biashara kabla ya kuanza biashara atakuwa na wajibu wa kuhakikisha:
(a) jengo lake limekaguliwa na Afisa Afya; na
(b) amepata kibali cha Halmashauri cha kufanya shughuli husika.

(2) Kibali cha kuendesha biashara ya nyumba ya kulala wageni, hosteli, shule, kituo cha kutolea huduma za afya au nyumba ya biashara kitatolewa baada ya Halmashauri kujiridhisha kuwa mahitaji yafuatayo yamezingatiwa: -

(a) jengo lina mwanga na hewa ya kutosha;
(b) jengo lina nafasi na vifaa vya kutosha;
(c) uimara wa jengo;
(d) jengo lina mfumo imara wa uondoshaji wa maji taka, miminika na taka ngumu;
(e) usafi wa jumla wa jengo na vifaa vyake;
(f) jengo lina vyoo na mabafu ya kutosha kwa jinsia zote;
(g) jengo lina vifaa vya zima moto;
(h) tanki la kuhifadhia maji safi;
(i) vyoo na bafu vimesakafiwa kwa vigae au marumaru na kuta zake zimewekwa vigae kiasi cha futi sita toka usawa wa sakafu;
(j) kwa nyumba za kulala wageni na hosteli, uwepo wa vyandarua.

(3) Mtu yeyote atakayekiuka masharti ya kifungu cha (1) atakuwa ametenda kosa.

(4) Bila kuathiri masharti ya kifungu cha (3), wakati wowote Halmashauri ikijiridhisha kuwa mmiliki hajakidhi masharti ya afya inaweza kuzuia utoaji wa huduma husika mpaka hapo mmiliki atakapokuwa amekidhi masharti ya kiafya yaliyotolewa na Halmashauri.

Upimaji wa afya

10. (1) Kila mmiliki wa hoteli, mgahawa, baa, bucha, sehemu za kuokea mikate, nyumba ya kulala wageni na grosari au mtu yeyote anayetengeneza chakula kwa ajili ya kuuza atatakiwa kuhakikisha mhudumu wake amepima afya kila baada ya miezi sita.

(2) Mmiliki yeyote atakayebainika kuruhusu mhudumu kufanya kazi bila kupimwa afya yake atatakiwa kulipa kiasi cha shilingi elfu hamsini na kuhakikisha mhudumu huyo anapimwa afya.

(3) Ada ya upimaji wa afya itakuwa shilingi elfu sita.

Ukaguzi wa afya.

11. Halmashauri itatoza ada ya ukaguzi wa afya kabla ya kutoa au kuhuisha leseni ya biashara.

Eneo la kutupa taka

12. (1) Halmashauri itakuwa na wajibu wa: -

(a) kutenga eneo maalum kwa ajili ya kutupia taka;

(b) kuweka vyombo maalum vya kutunzia taka katika maeneo ya Halmashauri; na

(c) kutoa huduma ya uzoaji taka kwa malipo kutoka kwa wazalishaji wa taka hadi kwenye dampo.

(2) Mtu yeyote atakayetupa taka au uchafu wowote au kuacha takataka au uchafu kwenye nyumba, uchochoro, kiwanja, mfereji wa maji ya mvua, barabara au mahali popote pasipotengwa kwa shughuli hiyo atakuwa ametenda kosa.

Vikundi vya wazoa taka

13. Halmashauri itahamasisha uundaji wa Vikundi Jamii na kuvitambua ili kuviwezesha kufanya shughuli za udhibiti wa taka ngumu pamoja na usafi wa mazingira katika mitaa baada ya kuingia mkataba na Halmashauri.

Magari ya abiria kuwa na vyombo vya kuhifadhia takataka

14. (1) Kila mmiliki wa gari la abiria litakaloingia katika eneo la Halmashauri atatakiwa kuwa na chombo cha kuhifadhi taka na kuhakikisha kwamba kila abiria anatupa taka kwenye chombo hicho.

(2) Endapo abiria atatupa takataka nje ya chombo cha usafiri, mmiliki au dereva au kondakta atawajibika kulipa kiasi cha shilingi elfu hamsini chini ya utaratibu wa kufifilisha kosa au kushtakiwa mahakamani.

Uhifadhi maji taka

15. (1) Kila mmiliki wa nyumba, kiwanda au eneo la biashara anatakiwa: -

(a) kuhakikisha kuwa analo karo la kuhifadhi maji taka;

(b) kunyonya maji taka pale karo linapojaa; na

(c) kutotiririsha au kutoelekeza maji kutoka vyooni, bafuni, karoni au viwandani kwenda barabarani, uchochoroni, mtoni, kwenye vyanzo vya maji, maeneo ya wazi, kwenye mfereji wa maji ya mvua au sehemu yoyote isiyotengwa kuhifadhia maji taka.

(2) Mtu yeyote atakayekiuka masharti ya kifungu kidogo cha (1) atakuwa ametenda kosa.

Ada ya utozaji taka

16. (1) Halmashauri itatoza ada ya uzoaji taka kila mwezi kutoka kwa kila kaya, wamilliki wa nyumba za biashara, taasisi na kampuni zilizopo ndani ya eneo la Halmashauri kwa viwango vilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hizi.

(2) Ada ya kila mwezi italipwa kila tarehe 30 ya kila mwezi ndani ya mwezi husika na italipwa kwa Afisa Mwidhiniwa ambaye atatoa stakabadhi ya malipo yatakayolipwa na atajaza katika rejista ya wazalishaji taka.

(3) Endapo mzalishaji wa taka atashindwa kulipia gharama ya huduma ya uzoaji taka kwa kipindi cha miezi miwili mfululizo, Halmashauri itamtaka kulipa deni hilo na adhabu ya asilimia hamsini ya ada anayostahili kulipa.

(4) Endapo mzalishaji taka atashindwa kulipa gharama ya huduma kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (3) itachukuliwa kuwa ametenda kosa chini ya Sheria Ndogo hizi.

Wajibu wa kuwa na choo na kukitumia

17. Kila mmiliki wa jengo la makazi au la biashara atakuwa na wajibu wa kuhakikisha kwamba jengo lake lina choo safi, imara na madhubuti na kuhakikisha kuwa kinatumika wakati wote.

Vyoo vya umma

18. Halmashauri inaweza kujenga vyoo vya umma au kumruhusu mtu binafsi, vikundi vya watu au taasisi kujenga vyoo vya umma vitakavyotoa huduma kwa malipo katika maeneo ambayo Halmashauri itaona kuwa kuna haja ya kufanya hivyo.

Vyoo vya muda katika mkusanyiko

19. (1) Mtu, kikundi au taasisi yenye lengo la kukutanisha watu kwa muda maalum katika eneo ambalo halina choo cha kudumu itatakiwa kujenga vyoo kwa matumizi ya wakati huo kwa idhini na usimamizi wa Halmashauri.

(2) Mtu, kikundi au taasisi itakayokiuka masharti ya kifungu kidogo cha (1) itakuwa imetenda kosa.

Ilani ya kujenga choo

20. (1) Endapo katika ukaguzi wa afya itagundulika kuwa nyumba yoyote haina choo, choo kilichopo kimejaa au hakifai kwa matumizi ya binadamu, Afisa Mwidhiniwa atatoa ilani ya siku thelathini kwa mmiliki wa nyumba akiainisha masharti ya kurekebisha hali hiyo.

(2) Mmiliki wa nyumba atakayeshindwa kutekeleza masharti ya Ilani iliyotolewa chini ya kifungu kidogo cha (1) atakuwa ametenda kosa.

(3) Bila kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1), Halmashauri inaweza kuamuru nyumba au jengo hilo lisitumike kwa shughuli za makazi au biashara hadi hapo hali hiyo itakapokuwa imerekebishwa.

Ilani ya kuondoa kero

21. (1) Endapo Afisa Mwidhiniwa atagundua kuwa eneo alilokagua lina kero yoyote atatoa ilani ya siku saba kwa mmiliki wa nyumba, mpangaji, mtumiaji au mtu yeyote anayehusika akimtaka kuondoa kero hiyo.

*Tangazo la Serikali Na. 712 (Linaendelea)*

(2) Mtu yeyote atakayeshindwa kutekeleza masharti ya ilani aliyopewa ndani ya muda ulioainishwa kwenye ilani atakuwa ametenda kosa.

Uteuzi wa Wakala

22. Halmashauri inaweza kuteua kampuni au kikundi cha jamii kutekeleza majukumu yake isipokuwa majukumu mahsusi ya Mkurugenzi, Afisa Mwidhiniwa na Afisa Afya chini ya Sheria Ndogo hizi.

Adhabu

23. Mtu yeyote atakayetiwa hatiani kwa kosa lolote chini ya Sheria Ndogo hii atahukumiwa faini isiyozidi shilingi elfu hamsini au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili au vyote kwa pamoja.

Kufifilisha kosa

24. Mkurugenzi anaweza kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa chini ya Sheria Ndogo hii kiasi cha shilingi elfu thelathini iwapo mkosaji atakiri kosa kwa hiyari na kuwa tayari kujaza fomu maalum iliyoambatishwa kwenye Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hizi.

## JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya kifungu cha 16 (1))*

Ada za uzoaji Taka

| Na. | Aina ya Biashara,asasi au kampuni | Ada kwa mwezi (tshs) | Ada kwa mwaka (tshs) |
|---|---|---|---|
| 1. | Kaya | 2,000 | 24,000 |
| 2. | Pombe za kienyeji | 5,000 | 60,000 |
| 3. | Maduka ya rejareja | 5,000 | 60,000 |
| 4. | Mama, baba lishe | 3,000 | 36,000 |
| 5. | Wachoma viazi/chipsi | 5,000 | 60,000 |
| 6. | Ghala za mbao | 5,000 | 60,000 |
| 7. | Restaurant (mgahawa) | 5,000 | 60,000 |
| 8. | Maduka ya jumla | 15,000 | 180,000 |
| 9. | Nyumba za kulala wageni | 10,000 | 120,000 |
| 10. | Mashine za kusaga/kukoboa nafaka | 5,000 | 60,000 |
| 11. | Viwanda vya mikate | 5,000 | 60,000 |
| 12. | Mashine za kuranda mbao | 15,000 | 180,000 |
| 13. | Ofisi za biashara na huduma | 4,000 | 48,000 |
| 14. | Maduka ya pombe za kigeni/grocery | 10,000 | 120,000 |
| 15. | Viwanda vya useremala | 10,000 | 120,000 |
| 16. | Saloon/vinyozi | 3,000 | 36,000 |

*Tangazo la Serikali Na. 712 (Linaendelea)*

| | | | |
|---|---|---|---|
| 17. | Gereji ya magari | 15,000 | 180,000 |
| 18. | Gereji ya pikipiki | 10,000 | 120,000 |
| 19. | Kuchoma mahindi` | 2,000 | 24,000 |
| 20. | Wauza barafu | 2,000 | 24,000 |
| 21. | Wauza kaseti na CD/DVD | 3,000 | 36,000 |
| 22. | Hoteli | 25,000 | 300,000 |
| 23. | Maduka ya nyama/bucha | 10,000 | 120,000 |
| 24. | Wachomeleaji/workshop welding | 10,000 | 120,000 |
| 25. | Watengenezaji wakubwa wa barafu | 5,000 | 60,000 |
| 26. | Wauza mkaa jumla | 15,000 | 180,000 |
| 27. | Wauza mkaa reja reja | 2,000 | 24,000 |
| 28. | Vituo vya kuuzia mafuta | 15,000 | 180,000 |
| 29. | Zahanati binafsi | 5,000 | 60,000 |
| 30. | Hospitali/vituo vya afya binafsi | 10,000 | 120,000 |
| 31. | Biashara ndogo ndogo zisizotajwa | 2,000 | 24,000 |
| 32. | Ghala za nafaka na bidhaa | 15,000 | 180,000 |
| 33. | Viwanda vikubwa vya nafaka | 30,000 | 360,000 |
| 34. | Shule/vyuo binafsi | 10,000 | 120,000 |
| 35. | Mafundi cherehani | 2,000 | 24,000 |
| 36. | Depo (TBL, COCACOLA/ PEPSI, SERENGETI, MAJI) | 20,000 | 240,000 |
| 37. | Kumbi za starehe na disco | 10,000 | 120,000 |
| 38. | Vibanda vya simu | 5,000 | 60,000 |
| 39. | Uchimbaji wa udongo na mawe kwa ajili ya matumizi ya viwandani au ujenzi. | 100,000 | 1,200,000 |
| 40. | Wauzaji wa ngozi | 10,000 | 120,000 |
| 41. | Viwanda vidogovidogo | 15,000 | 180,000 |
| 42. | Umwagiliaji wa mashamba kutoka maji ya mito ya asili | 15,000 | 180,000 |
| 43. | Viwanda vya kuchakata nafaka | 20,000 | 240,000 |
| 44. | Sehemu za kuoshea magari/Car wash | 30,000 | 360,000 |
| 45. | Nyumba za kufua nguo/Dry cleaner | 15,000 | 180,000 |
| 46. | Maduka ya madawa (pharmacy) | 7,000 | 84,000 |
| 47. | Maduka ya madawa muhimu (DLDM) | 4,000 | 48,000 |
| 48. | Studio za picha | 15,000 | 180,000 |
| 49. | Wauzaji wa miwa na matunda | 9,000 | 108,000 |
| 50. | Biashara nyingine zisizotajwa | 5,000 | 60,000 |
| 51. | TTCL | 10,000 | 120,000 |
| 52. | BENKI | 10,000 | 120,000 |
| 53. | POSTA | 10,000 | 120,000 |

*Tangazo la Serikali Na. 712 (Linaendelea)*

| | | | |
|---|---|---|---|
| 54. | TANESCO | 10,000 | 120,000 |
| 55. | TANROAD | 10,000 | 120,000 |
| 56. | MINARA YA SIMU | 10,000 | 120,000 |
| 57. | MAJENGO YENYE OFISI NYINGI | KILA OFISI KULIPIA TOZO | |
| 58. | Na mengine yatakayoanzishwa | 10,000 | 120,000 |

JEDWALI LA PILI

*(Limetungwa chini ya kifungu cha 24)*

HATI YA KUFIFILISHA KOSA

Mimi……………………. nakiri KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya …………………………ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Mpanda, kuwa Tarehe ………Mwezi………. Mwaka………. nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kifungu cha………………. cha Sheria Ndogo za Afya na Usafi wa Mazingira za Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda za Mwaka 2020.

Kwa mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri, niko tayari kulipa kiasi cha shilingi elfu thelathini na kutekeleza wajibu wangu badala ya kushitakiwa mahakamani.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI KWELI NA NINAYATOA KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU

Leo tarehe………………………………. ya Mwezi…………………. Mwaka…………………

Jina………………………………………Saini……………………………… ………

Mbele ya:

Jina……………………………………...Cheo……………………………… …….

Saini……………………………………Tarehe……………………………… ……

Lakiri ya Halmashauri ya Manispaa Mpanda imegongwa katika Sheria Ndogo hizi kufuatia azimio Na: MUHT/MMC/BARAZA/02/2018/2019/AGD:13 la kikao cha Halmashauri ya Manispaa Mpanda kilichofanyika tarehe 25 Mwezi Januari,2019, na imebandikwa na kushuhudiwa na;

MICHAEL F. NZYUNGU
*Mkurugenzi,*
*Halmashauri ya Manispaa Mpanda*

WILLIAM P. MBOGO
*Mstahiki Meya,*
*Halmashauri ya Manispaa Mpanda*

L.S

NAKUBALI,

Dodoma,
5 Agosti, 2020

Mhe. SELEMANI S. JAFO (Mb)
*Waziri Wa Nchi- OR - Tamisemi*